



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA FEDHA**  
**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

Zanzibar, 31 Agosti, 2023

**WAFANYAKAZI 166 WA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO  
WALIPWA MAFAO YA BIMA YA GEAS**

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) imepokea mafao ya Bima ya Group Endowment Assurance Scheme (GEAS) kwa watumishi wake **166** ambao walikuwa wamekata bima ya mfuko wa maisha inayotoa mafao kwa wafanyakazi wake wanapostaafu au kufariki. Watumishi hao walikata bima kupitia kampuni ya ushauri wa bima iitwayo **Intertrade Express Limited** ambayo ni wakala wa Shirika la Bima la Taifa (NIC).

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, malipo ya mafao ya awamu ya kwanza yalifanyika mwezi Desemba 2022, awamu ya pili mwezi Machi 2023, na awamu ya tatu mwezi Agosti 2023.

Malipo haya ni matokeo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamishina wa Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware kulipa wanufaika wote wa skimu ya bima ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa mujibu wa mkataba na makubaliano ya pande zote yaliyofanyika tarehe 09 Juni 2022.

Baada ya kupokea malalamiko kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Kamishina wa Bima aliunda kamati maalum iliyojumuisha wajumbe kutoka TIRA, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, NIC na Kampuni ya Ushauri wa Bima ya Intertrade ambao wote ni wahusika katika swalala hilo.

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetoa shukrani zake za dhati kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa ushirikiano walioutoa katika kuhakikisha watumishi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wanalipwa mafao ya GEAS.

TIRA ikiwa ni Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Bima itaendelea kuhakikisha haki za wanufaika wa bima mbalimbali zinalindwa na kupatikana kwa wakati. Mamlaka inawasihi Watanzania kuendelea kutumia huduma za bima nchini na kutosita kuleta malalamiko yao kwa Kamishna wa Bima pindi wanapoonza kampuni za bima haziwatendei haki kwani Kamishna wa Bima amepewa mamlaka kupitia **Sheria ya Bima SURA Na. 394**, kutoa adhabu kwa mtu yeyote, Kampuni au taasisi itakayobainika kuvunja Sheria ya Bima.

Imetolewa na;



Hadija Maulid  
Meneja Mahusiano na Mawasiliano  
**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA**

**OFISI ZA TIRA MAKAO MAKUU:**

JENGO LA LAPF, Ghorofa ya 5, Mtaa wa Makole, S.L.P 2987, DODOMA, Tanzania, Simu: +255 26 2321180, Nukushi: +255 26 2321180, Barua pepe: cor@tira.go.tz

**Ofisi za Zanzibar:**

Jengo la TIRA, Mtaa wa Kilimanj, S.L.P 133 Zanzibar, Simu: +255 242237271, Nukushi: +255 24 2237272, Tovuti: [www.tira.go.tz](http://www.tira.go.tz), Barua pepe: dcoi@tira.go.tz